**Miaka 50 ya Muungano na udhibiti wa uhamiaji haramu nchini.**

(Na Immaculate Makilika)

Tarehe 26 Aprili, 2014 Watanzania tanashuhudia Muungano wetu ukitimiza nusu karne. Miaka hii 50 ya Muungano imekuwa ni yenye mafanikio makubwa ambayo yamenufaisha wananchi katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Muungano umewapa fursa wananchi wa pande zote mbili kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote walipo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili linadhihirisha kuwa Muungano wetu umeendelea kuwa nyenzo na utambulisho muhimu wa umoja wetu.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Taasisi zake husika za Muungano kwa kushirikiana na wananchi zimeendelea kudhibiti matishio ya kiusalama yanayojitokeza na kuimarisha amani iliyopo. Mfano, udhibiti wa tatizo la uhamiaji haramu nchini. Huku tukishuhudia kukua na kuongezeka kwa biashara na uwekezaji, utalii na miradi mbalimbali ya kimaendeleo kutokana na hali ya amani na utulivu uliopo.

Lakini je, mhamiaji haramu ni nani? Ifahamike kuwa ni mtu yeyote aishie ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isivyo halali na sheria na taratibu za nchi.

Uhamiaji haramu ni tatizo linalozikumba nchi nyingi dunia,na madhara yake ni makubwa hasa kama nchi husika haitachukua hatua za maksudi za kuzuia tatizo hili.Tanzania ni nchi mojawapo inayokumbwa na tatizo hili ukizingatia kwamba imezungukwa na mataifa kadhaa kama Rwanda,Burundi,Kenya,Malawi,Msumbiji, DRC Congo na baadhi ya mataifa hayo yamekua kwenye vita kwa muda mrefu, hali inayosababisha wananchi wake kukimbilia mataifa mengine ili waweze kupata hifadhi.

Katika miaka ya hivi karibuni tatizo la uhamiaji haramu limeongezeka kwa kasi nchini hivyo na kusababisha vyombo husika kukabiliana na hali hiyo. Idara ya Uhamiaji ni moja ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama vyenye jukumu la kuhakikisha kwamba Ulinzi na Usalama wa nchi unaimarishwa. Katika kusimamia jukumu hilo kikamilifu, Idara ya Uhamiaji inatekeleza majukumu makuu ya Msingi yafuatayo: Kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu

nchini, kutoa huduma ya pasipoti au hati nyingine za safari kwa Watanzania wanaosafiri nje ya nchi kwa shughuli mbalimbali, kutoa huduma ya vibali vya kuishi nchini pamoja na Pasi mbalimbali kwa wageni wanaokuja nchini kwa shughuli mbalimbali, Kufanya misako, doria, kubaini na kuwakamata wahamiaji haramu nchini na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria zilizopo pamoja na kuratibu mchakato wa maombi ya wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

Majukumu hayo ndiyo yanaipatia Idara ya uhamiaji wajibu wa kulinda na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi, sambamba na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama.Lakini je hali ilikua vipi kabla na baada ya kukumbwa ha tatizo hili la uhamiaji haramu katika maeneo mbalimbali nchini?

Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Kiziramuyaga,Mleba Mkoani Kagera Zephrine Tibekebuka,ameelezea athari nyingi zilizotokana na wimbi la wahamiaji haramu kijijini kwake "vyanzo vya maji vimeharibiwa,ukataji miti ulikithiri na ujambazi ulikua ukitishia uhai wetu ikiwemo na utekaji magari" hata hivyo amekiri kuwa mara baada ya zoezi la kuwataka wahamiaji hao warudi makwao angalau sasa hali imekua shwari na kusema japo si kama ilivyokuwa hapo awali.

Hali kadhalika,Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu Mkoa wa Mtwara Festo Kiswaga, kwa upande wake anasema pamoja na kuwa mkoa wa Mtwara ni kati ya mikoa iliyopo pembezoni huku daraja la Umoja Masasi ndio lilitumika kuvusha hao wahamiaji haramu kwenda Msumbiji kwa muda wa miaka mitano kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kudhibiti tatizo hili .Aliendelea kwa kusema kuwa "kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya imekua ikitoa taarifa za mara kwa mara juu ya wageni au wahamiaji haramu hapa wilayani,elimu imekua ikitolewa katika kila kijiji juu ya uhalifu na uhamiaji haramu na hali hiyo kupelekea wahamiaji hao hasa toka Ethiopia,Sudan na wachache toka Rwanda na Burundi kupungua kwa kiasi kikubwa" alisema Kiswaga.

Kwa upande wake Marium Salum mkazi wa Kiembe Samaki mjini Unguja huko Zanzibar, yeye amesema anafurahishwa sana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Muungano katika kuhakikisha wahamiaji haramu wanarudishwa makwao "kusema ukweli serikali yetu ya Muungano inafanya kazi kubwa haswa katika hili,na mie nafurahi kwa hilo" alisema Marium

Akizungumza katika  ziara iliyoanza Julai 24, mwaka 2013 katika Mkoa wa Kagera pamoja na  uzinduzi wa miradi tisa ya maendeleo  Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya Kikwete alikemea tatizo la uhamiaji haramu nchini na kusema kuwa “Kuna baadhi ya Wenyeviti wa vitongoji na vijiji wamejigeuza maafisa uhamiaji wa serikali na kutoa vibali kwa wahamiaji”

Hii ni kutokana na ukweli kuwa, baadhi ya wahamiaji haramu wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya uhalifu wa kutumia silaha (ujambazi na utekaji) pamoja na uharibifu wa mazingira hivyo, wazo la kuwarejesha makwao na kuwabaini wanaowakaribisha na kuwatunza kwa namna yoyote kuchukuliwa hatua za kisheria, halina budi kutekelezwa kwa nguvu huku  rais akisema kuwa uhamiaji haramu  kweli ni ugonjwa unaohitaji dawa mapema.

Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na tatizo la uhamiaji haramu nchini,Serikali ilianzisha operesheni maalumu iliyopewa jina la ‘Operesheni Kimbunga’ kwa lengo la kuwaondoa nchini watu wote ambao hawana uraia au haki ya kisheria kuishi nchini.

Naibu Kamishna wa Polisi nchini Kamanda Simon Sirro alisema katika kipindi cha Operesheni Kimbunga Awamu ya Pili jumla ya wahamiaji haramu 425 walikamatwa wakiwemo watu 5 wanao tuhumiwa kwa kosa la kuwahifadhi na kuwatorosha wahamiaji haramu.

Miongoni mwa wahamiaji haramu waliokamatwa ni Warundi 180, Wanyarwanda 149, Waganda 82 na Wakongo 14. Mkoa ambao unaongoza kwa kukamata wahamiaji haramu wengi ni Kagera (209), Kigoma (166) na Geita (50).

Aidha, Majangili 11 walikamatwa pamoja na meno ya Kiboko na Ngozi ya Mbwea. Jumla ya Makokoro 12, Bangi kilo Tatu, Gongo Lita271 na Magunia ya Mkaa 100 yaliyotengenezwa kwa mazao ya misitu kinyume na Sheria vilikamatwa katika mikoa ya Kagera, Kigoma na Geita.

Hali kadhalika wakati wa Operesheni Kimbunga awamu ya Pili katika mikoa ya Kagera, Kigoma na Geita  jumla ya Ng’ombe 2,220 walikamatwa kwenye hifadhi ya Taifa kwa kipindi cha siku 10 tangu kuanza kwa awamu hii ya operesheni Septemba 21, 2013.

Kwa mujibu wa Kamanda Sirro, jumla ya watuhumiwa 88 wa unyang’anyi wa kutumia silaha pamoja na silaha 23 zikiwemo Bomu la kurushwa kwa mkono Moja, bunduki aina ya SMG 3, Pisto 2, Magobole18 na Risasi 484 miongoni

mwake zipo risasi za SMG/SAR 471 na risasi za Pisto 13, magazine za SMG 2 na Sare za Jeshi la Burundi zilikamatwa katika kipindi cha siku 10 za operesheni Kimbunga Awamu ya Pili.

Aidha Mbunge wa Kasuli mkoani Kigoma,Moses Machali,ameeleza kuwepo kwa athari zilizotokana na wahamiaji haramu kwenye eneo lake na kusema kuwa kumekuwepo na matatizo ya uhalifu wa kutumia silaha, uharibifu mkubwa wa mazingira,na hata masuala ya kiafya yamekuwa ni changamoto kwa kuwa na mrundikano wa watu wengi katika eneo moja aliongeza kwa kusema kuwa uwepo wao umeongeza gharama hata kwa Serikali, huku akiomba Serikali kushirikisha wananchi zaidi.Pia mwandishi wa makala hii alifanya mahojiano na mwananchi wa kijiji cha Nkwenda Mkoani Karagwe,Agustine Rweyemanu yeye kwa upande wake ameleza jinsi alivyopoteza mazao yake baada ya kuharibiwa vibaya na mifugo ya watu waliohitaji malisho lakini na kuharibiwa vyanzo vya maji na kupelekea kupata hasara kubwa.

Afisa Afya Mazingira Deogratias Nazareno,anasema madhara yanayoweza sababishwa na wimbi la uhamiaji haramu ni pamoja na kuwepo na idadi kubwa ya wanyama kuliko uwezo wa maeneo husika na hali hiyo husababisha mmomonyoko wa udongo,kuharibu uoto wa asili na shughuli za kilimo,uharibifu wa vyanzo vya maji,mara nyingine silaha hutumika kuulia wanyama na kuongeza kuwa wanyama ni sehemu ya mazingira.

“Matumizi sahihi ya kilimo na ufugaji hasa maeneo yaliyoathiriwa na wahamiaji haramu kama Bunanzi,Karagwe na Ngimbe inafaa yatiliwe mkazo zaidi” alisema Nazareno.

Kama ambavyo rais kikwete anasema si kwamba hawataki watu kuchukua uraia na kuukana uraia wanchi yao la hasha bali wafuate utaratibu na nchi wasiibalidi kama shamba la bibi ya kila mtu anaingia na kutoka jinsi anavyojisikia.Pia ikumbukwe kwamba Tanzania kama taifa huru imefanya kazi kubwa ya kutoa hifadhi ya watu ambao vita imewalazimu kuzikimbia nchi zao na kutafuta hifadhi kama wakimbizi.

Aidha, Tanzania imesaini Refugee Act ya mwaka 1998 inayotanabaisha kinagaubaga kuhusu usalama wa wakimbizi na namna gani ya kuishi wawapo nchini.Hii ni kwa kuzingatiia kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua haki za binadamu na mahitaji mengine ya msingi yanayomuwezesha binadamu huyo aishi kwa amani.

Aidha, mwaka 1994 yalitokea mauaji ya halaika huko nchini Rwanda na kupelekea mamilioni ya raia wa Rwanda kukimbilia Tanzania.Lilikuwa jukumu la serikali ya Tanzania kuwatunza kwa kuwapatia hifadhi watu wote hao kwenye kambi mbali mbali nchini.

Mwakilishi wa UNHCR nchini Bibi.Joyce Mends-Cole wakati wa maadhimisho ya siku ya wakimbizi Duniani alieleza kuwa, takribani raia wa Burundi 170,000 walioingia Tanzania mwaka 1972 kama wakimbizi na kuruhusiwa kuishi mikoa ya Tabora na Katavi wamekua wakisubiri hatua za mwisho za kupatiwa uraia wa Tanzania tangu mwaka 2010.Hii itawaruhusu kupata haki zao katika nchi waloyokuja kuipenda na kuichukulia kama nchi yao.

Pamoja na kuwa Serikali ya Jamhuri wa Muungano Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti tatizo la uhamiaji haramu nchini,aidha Katika kipindi cha miaka hamsini ya Muungano, Idara ya Uhamiaji imefanikiwa kuwa na jengo jipya la kisasa kwa ajili ya Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu jijini na Dae es Salaam na Jengo Jipya la Idara ya Uhamiaji Zanzibar likiwa katika maeneo ya Kilimani.

Halikadhalika kumekuwa na Mfumo wa utoaji VISA uliofungwa katika vituo vya kuingia na kutoka nchini na katika Ofisi zote za Balozi za Tanzania nje ya nchi. Idara kwa kushirikiana na UNHCR imefanikiwa kuweka mfumo wa kisasa wa elektroniki kwa ajili ya kuchapisha na kutunza kumbukumbu za Vyeti vya Uraia wa Tajnisi (Citizenship by Naturalization Certificates) ikilinganishwa na vile vilivyokuwa vinatolewa hapo awali kwa mfumo wa kizamani “manual” na hivyo kuwa rahisi kughushiwa.

Hakika Muungano wetu umesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti tatizo la uhamiaji haramu nchini, witoooo kauli mbiu ya muungano ya mwaka huu.

Jengo Jipya la Idara ya Uhamiaji Zanzibar likiwa  katika maeneo ya Kilimani ( kiinuwa miguu) jirani na jengo la zamani.

Mwisho